

KATIKA NURU YAKE YA AJABU

Mafundisho ya Biblia

"Mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika Nuru yake ya ajabu"
1 Petro 2:9

"Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako."
Zaburi 119:18

UTANGULIZI

Unapotoka katika chumba chenye giza na kuingia sehemu yenye juu, mwanga unaweza kukufanya ushindwe kuona. Macho yetu yanapoanza kuzoea mwanga tunaweza kuona vyema zaidi na kufurahia sura inayotzunguka. Vivyo hivyo tunapotazama katika nuru ya maandiko, mng'ao wa ukweli wakati mwingine unaweza kuumiza. Walakini macho yetu ya kuona ya kiroho yanavyobadilika basi tunaweza kufurahia "kutembea nuruni".

Somo hili la kujifunza Biblia limetayarishwa ili kutuwezesha sisi "kutembea" katika nuru ya ajabu ya Neno la Mungu. Katika kufanya hili, tutakuwa waangalifu katika "ukitumia kwa halali neno la kweli" (2 Timotheo 2:15) kwa kuzama katika mwanga wa juu wa migawanyiko mitatu ya mpangilio wa miaka ya Agano Jipyia pamoja na:

1. INJILI - Zikiwa na maneno na kazi za Yesu.
2. MATENDO YA MITUME - Kuelezea matendo na mahubiri ya Mitume.
3. NYARAKA - Zinaonyesha barua zote zilizoandikwa na Mitume kwa

makanisa waliyoanzisha katika kitabu cha Matendo.

Tunaamini kuwa maandiko yote yamevuvuviwa, na "hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu" (2 Petro 1:20-21). Kwa hiyo kila jitihada imefanyika katika kuleta Neno halisi la Mungu pasipo kuongeza au kupunguza mafundisho yake (Kumbukumbu la Torati 4:2; Mithali 30:5-6). Kwa kukiri Biblia kama mamlaka yetu pekee ambayo kila mmoja wetu anaweza kuamini kwa wokovu wetu, kwani ni Neno la Mungu ndilo litakalituhukumu wote siku ile ya mwisho.

Hebu tusome 2 Timotheo 3:15-16 tunapoanza safari yetu kwenye Neno la Mungu.

KATIKA INJILI

Yohana 1:1-5 & 14

Hapo mwanzo, _____ alikuwa na akafanyika mwili.

Yesu Kristo ni Neno Hai la Mungu.

Yohana 1:11-13.

Kama tukimwamini na kumpokea, Yesu anatupa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu _____ kwa kuzaliwa ambako siyo uzao ule wa kawaida. Alizungumza zaidi kuhusu kuzaliwa mara ya pili usiku mmoja kwa yule mtawala wa Wayahudi.

Yohana 3:18

Bwana alimwambia Nikodemo kuwa mtu anayetaka kuuona au kuingia katika ufalme wa Mungu ni lazima azaliwe mara ya pili kwa _____ na kwa _____.

Yohana 3:16-21

Yesu alimwambia Nikodemo pia kuwa kila _____ atakuwa na uzima wa milele. Yesu alitaja kama mambo mawili tofauti yanayotakiwa kwa wokovu, moja ni kuzaliwa mara ya pili, nyingine ni kuamini. Hata hivyo hii siyo kwamba

yanapingana. Andiko linalofuatia linaeleza jinsi kuamini kunavyohusiana na kupata tendo la kuzaliwa kwa Roho.

Yohana 7:38-39

Hapa, tunagundua kuwa kama tukimwamini Yeye (kama yanenavyo Maandiko), tutapokea _____. Tunaona kuwa kuamini kimaandiko ni bora zaidi kuliko kubadili jinsi tunavyodhania. Na pia inaleta matokeo ya kimaandiko.

Yohana 12:35-36 & 42-43

Leo, kama siku zile za Yesu, wengi wanamwamini yeye. Lakinii hawataacha kwa kuogopa yale ambayo wengine watakayofanya au kuyasema.

Yohana 12:44-48 (1)

Katika kujibu hofu zao, Yesu alionya kuwa _____ lake ndilo litakalotuhukumu, kwa hiyo ni lazima tuwe waangalifu tusije tukalikataa. Badala yake tuliamini na kulitii pasipo kujali wengine wanafanya nini au wanasema nini!

Yohana 17:17-20 (2)

Katika maombi ya Yesu kwa ajili ya wanafunzi wake, kabla ya kusulubiwa kwake, alisema Neno la Mungu ndilo . Alituombea pia sisi na wale wote watakaomwamini kwa kupitia neno la Mitume.

Kupata neno la Mitume lilikuwa nini? hebu tusome kile Yesu alichowaambia kutangaza. Katika kuweka agizo kuu lililokuwa likifuatia katika andiko la Luka 24:45-49 (3) mara baada ya kifo cha Bwana, kuzikwa na kufufuka...na kabla ya kupaa kwake mbinguni.

"Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu: na kwamba mataifa yote yatahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanzia tangu Yerusalem. Nanyi ndinyi mashahidi wa

mambo haya. Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu, lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu."

**JE! MITUME WALIHUBIRI UJUMBE
AMBAO YESU ALIWAAGIZA
KUTANGAZA?**

**JE! AHADI YA BABA
ILITIMIZWAJE?**

Hebu tuendelee na safari yetu katika Neno la Mungu kwa kuangalia ni nini kilichohubiriwa na ni nini kilichotokea kule Yerusalemu.

KATIKA MATENDO YA MITUME

Matendo 1:3-5

Tunapoingia katika kitabu cha Matendo tunagundua mara moja kuwa ahadi ya Baba ilikuwa ni ubatizo wa _____.

Matendo 2:1-17.

Wakati Mitume walipokuwa Yerusalemu pamoja na wengine wengi, kwa furaha walijazwa Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka.

Watazamaji na wale waliokuwa wakishangaa kutoka katika mataifa mengi waliposikia wakinena kwa lugha nyingine waliuliza "maana yake ni nini Mambo haya?" Ndipo Petro alipoeleza ahadi ya kuja kwa Roho na kuendelea kumhubiri Kristo na mpango halisi wa Wokovu wa kimitume.

Matendo 2:36-39.

Wakati watu walipomsikia Petro maneno yake waliamini kuwa Yesu Kristo alikuwa Bwana wao na Mwokozi wao, waliskitika kwa ajili ya dhambi zao na wakamuuliza Petro na mitume wengine kuwa wanatakiwa wafanye nini. Petro alijibu kwa kuhubiri ule ujumbe alioamuru Yesu kuwa uhubiriwe katika Luka 24:45-49. Katika mwanga wa hili, anaangalia mambo matatu ya mpango wa wokovu ambao Petro aluhubiri katika mstari wa 38:

- 1. TOBA
- 2. ONDOLEO LA DHAMBI
KUPITIA UBATIZO WA JINA
LA YESU
- 3. KUPOKEA KIPAWA CHA
ROHO MTAKATIFU

ONA: Matendo 2:38 ni kutimiza mambo yale yote mawili ya kuzaliwa mara ya pili yaliyotajwa na Yesu katika Yohana 3:5 kuwa yalikuwa ni muhimu ili kuweza kuingia katika ufalme wa Mungu! Kuzaliwa kwa maji = ubatizo katika Jina la Yesu Kristo kuzaliwa kwa Roho = Kujazwa Roho Mtakatifu! Sasa, hebu tuangalie mifano mingine zaidi ya watu kuzaliwa mara ya pili kwa maji na kwa Roho kama Neno ambalo Yesu aliwapa wanafunzi wake lilivyokuwa likiendelea kuhubiriwa katika kitabu chote cha Matendo ...

FILIPO ANAHUBIRI KWA WASAMARIA MATENDO 8...

TAZAMA: Watu wengine wanasema wanapoona furaha au wanapomwamini Yesu, au walipobatizwa basi moja kwa moja walijazwa Roho Mtakatifu. Lakini Neno linasemaje?

Matendo 8:5-8 Je walikuwa na furaha kuu?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari wa 12 Je walimwamini Yesu?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari 14-17 Je walibatizwa katika Jina lake? Ndiyo ____ Hapana ____

Je walipokea Roho Mtakatifu kama kitu tofauti na tukio halisi?

Ndiyo ____ Hapana ____

PETRO ANAHUBIRI KWA MATAIFA MATENDO 10...

TAZAMA: Watu wengine wanasema kuwa na dini inatosha, au ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa ishara ya kunena kwa lugha

ilikuwa ni siku ile ya Pentekoste peke yake. Kama Biblia inasema hivyo basi ni kweli. Lakini kama Biblia haisemi hivyo kwa kupitia Kornelio kwa tukio ililotokea basi hiyo siyo kweli.... Basi ni hapana.

Matendo 10:1-2 - Je Kornelio alikuwa mwenye dini?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari 5-5 - Je Mungu alikuwa na mengine kwa Kornelio kuyafanya?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari 44-46 - Je walipokea Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha nyingine baada ya Pentekoste?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari 47-48 - Je waliendelea kubatiza katika Jina la Yesu?

Ndiyo ____ Hapana ____

PAULO ALIWAHUBIRIA WANAFUNZI WA YOHANA MATENDO 19...

TAZAMA: Watu wengi amba ni waamini amba wala hawajasikia kuhusu Roho Mtakatifu ambaye aliahidiwa kwao. Pia, wengine husema siyo muhimu kubatizwa au kubatizwa tena. (Kama ungekuwa umebatizwa na Yohana Mbatizaji, je unadhani ingekuwa ni muhimu kubatizwa tena kwa kutumia mfumo mwingine tofauti wa ubatizo?) Wengine wanasema usijali kuwa ni nini kilichozungumzwa unapobatizwa kama Biblia ingeonyesha kuwa hakuna neno basi ni sawa. Lakini ...itakuwaje kama Biblia inaonyesha kuwa ni kitu cha kujali?

Matendo 19:1-2: Walikuwa ni waamini, lakini je walikuwa wamesikia au kupokea Roho Mtakatifu?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari wa 3-7 Wale walibatizwa na Yohana walibatizwa tena kwa Jina la Yesu?

Ndiyo ____ Hapana ____

Mstari wa 6 Kupokea Roho Mtakatifu kulifuatana na kunena kwa lugha?

Ndiyo ____ Hapana ____

Tumeona kuwa Mitume walihubiri ujumbe wa wokovu ufuataao"

- Maisha ya Kristo na kifo
- Toba kumwelekea Mungu na amini katika Kristo Yesu.
- Ubatizo katika maji kwa
- Upokeaji wa Roho Mtakatifu (uliofuatana na ishara ya

Sasa, hebu tusome Mitume walikuwa na nini la kusema kuhusu ujumbe wa wokovu waliouhubiri katika kitabu cha Matendo. Tunaweza kwa kusoma Nyaraka (barua) walizowaandikiakwa ajili ya waokovu wao.

KATIKA NYARAKA

Tutakapokuwa tukisoma Nyaraka, tutaona ni jinsi gani Mitume walivyojisikia kuhusu Injili (habari njema) za wokovu. Hii siyo kwa sababu walikuwa werevu sana. Ni kwa sababu walijua Neno la Yesu lilitolewa kwa kulihubiri na ndilo litakalienda kuwahukumu watu wote.

Petro alisema nini?

"Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli...kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili...kwa neno la Mungu...Na neno hilo ni neno lile jema lilohubiriwa kwenu".
(1 Petro 1:22-25).

Kulitii Neno la Mungu kunatakasa roho zetu.

Petro aliuliza swali:

"... Mwisho wao wasioitii Injili ya Mungu utakuwaje?" (1 Petro 4:17-18).

Paulo alitoa jibu:

"Wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake; katika mwali wa moto huku akiwalipiza kisasi wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Watakaoadhibiwa na maangamizi

ya milele kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake" 2 Thesalonike 1:7-9.

chake, maziko na ufufuo.

Ni umuhimu wa milele kuitii Injili!

Zalihiswa katika Jina la Yesu.

"Nastaajabu kwa kuwa mnawacha upesi kuhesa kwa lugha nyingine. hivi ye ye aliye wai ta katika neema ya Kristo, na kugeukia Injili! ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza Injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi Injili yoyote alaaniwe. Kama tuliviyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo mliyo ipokea na alaaniwe." (Wagalatia 1:6-9).

Yakobo anasemaje?

"... Na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana huijiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo." (Yakobo 1:21-24).

Neno linawenza kuokoa roho zetu!

***YAKOBO ANATUAMBIA KWAMBA KAMA
TUKIONA KITU TUNACHOHITAJI
KUFANYA, TUTAKAVVOKUWA
TUKIJITAZAMA KWENYE "KIOO CHA
NENO" BASI TUFANYE. HEBU
TUAMUE SASA TUTAFANYA NINI
KWA YALE YALIYO MBELE YETU.***

**MAANDIKO YA NYONGEZA YA
KUJIFUNZA**

1. Mathayo 7:13-24

TAZAMA: Onyo la Mungu kuhusu manabii wa uongo na kuwa watendaji wa neno na siyo wasikiaji tu wa Neno.

2. Mathayo 16:15-19

TAZAMA: Petro alipewa "funguo za ufalme" kwa sababu ya ufunuo wake kuhusu Yesu alikuwa nani:

3. Maandiko mengine ya "Agizo Kuu":

TAZAMA: Katika Mathayo 28:18-20 Neno "jina" ni umoja katika agizo hili la kubatiza. Mitume walitii agizo hili walipobatiza tu katika jina la Yesu, na siyo kwa kutumia vyeo viliviyotajwa hapa. (angalia Matendo 4:12)

4. Marko 16:15-18. Umuhimu wa ubatizo na ishara kufuata waaminio.

5. Matendo 8:35-39

TAZAMA: Filipo ni lazima alikuwa ametaja ubatizo wakati alipomhubiri Yesu Kristo kwa yule Towashi wa Kushi, kwa sababu yule Towashi alimwambia ambatize katika maji. Neno la Kiyunani la kubatiza ni "baptiso" lenye maana halisi "kufunika kabisa na maji kuzamisha" (tazama pia Warumi 6:3-5).

Mathayo 16:15-19

TAZAMA: Petro aliyepewa "funguo za ufalme" alizitumia kwa kufungua "mlango wa ufalme kwa kuhubiri ujumbe halisi wa kimitume wa wokovu kwa mara ya kwanza.

6. Matendo 10:34-43

TAZAMA: Petro alihubiri maisha na U-Bwana wa Yesu Kristo, vile vile Kifo chake, mazishi na ufufuo wake.

7. I Petro 3:20-21

TAZAMA: Kufuatana na Petro, ubatizo ni muhimu katika sehemu ya wokovu.

*Tunakutia moyo kusoma Injili zote,
Matendo ya Mitume na Nyaraka kwa undani
zaidi ... na kuendelea kutembea ... Ndani ya
Nuru yake ya ajabu"*

MWISHO

JE UNAAMINI: Neno la Mungu kuwa ni kweli na litatuhukumu?

JE UNAAMINI: Kuwa Yesu Kristo ni Bwana na Mwokozi?

JE UNAAMINI: Kuwa ni muhimu kutubu na kuamua kugeuka kutoka katika dhambina kutoa maisha yako kwa Mungu?

JE UNAAMINI: Kuwa ubatizo wa Jina la Yesu Kristo ni njia ya Biblia ya kubatizia?

JE UNAAMINI: Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili yako leo na utakapompokea utanena kwa lugha nyingine kama vile walivyofanya katika Biblia?

**KAMA UNAAMINI MAMBO
HAYA, OMBA SASA NA
KUMWOMBA MUNGU
KUKUWEZESHA KUYAONA
YALE YOTE ALIYONAYO KWA
AJILI YAKO!**